

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS



### MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

#### TAARIFA KWA UMMA

#### WANANCHI NA WADAU KUTOA MAONI KUHUSU MPANGO KAZI WA KITAIFA WA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI WA AWAMU YA TATU 2016/17-2017/18 (NATIONAL OPEN GOVERNMENT PARTNERSHIP-ACTION PLAN III)

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (**Open Government Partnership – OGP**) kuanzia mwaka 2012. Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) ni jitihada za kimataifa katika kuhimiza uendeshaji wa Serikali kwa uwazi zaidi, ushirikishwaji mkubwa wa wananchi, kudhibiti rushwa katika jamii na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa umma.

Moja ya Vigezo na Matakwa ya utekelezaji Mpango huu kwa nchi mwanachama ni kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa (**National Action Plan**) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi.

Rasimu ya Mpango Kazi (**National OGP Action Plan**) kwa mwaka 2016/17-2017/18 imeandaliwa. Mpango Kazi huo, utahusisha vipaumbele katika maeneo saba ambayo ni **Upataji Taarifa (Access to Information)**, **Takwimu Huria (Open Data)**; **Bajeti za Wazi (Open Budget)**; **Uwazi kuhusu Ardhi (Land Transparency)**; **Uwazi kuhusu Tasia ya Uziduaaji (Extractive Industries Transparency)**; **Uwazi katika Masuala ya Afya (Medical and Health Service Transparency)**; na **Mifumo ya Utendaji Kazi (Performance Management Systems)**.

Hivyo, Serikali inawakaribisha Wananchi na wadau kutoa maoni na ushauri ili kuiboresha Rasimu ya Mpango Kazi wa Kitaifa (**National Action Plan**) hususan katika maeneo yenye upungufu ili kuuboresha zaidi. Njia zitakazotumiwa na wananchi na wadau kuwasilisha maoni yao ni Tovuti Rasmi ya Wananchi ([www.wananchi.go.tz](http://www.wananchi.go.tz)), Tovuti ya OGP ([www.opengov.go.tz](http://www.opengov.go.tz)), **Government Open Data Portal** ([www.opendata.go.tz](http://www.opendata.go.tz)), kupitia barua pepe ([ps@utumishi.go.tz](mailto:ps@utumishi.go.tz)) ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa njia ya barua kupitia **S.L.P. 2483, Dar es Salaam**.

Rasimu ya Mpango Kazi huo inapatikana katika Tovuti ya Wananchi ([www.wananchi.go.tz](http://www.wananchi.go.tz)), Tovuti ya OGP ([www.opengov.go.tz](http://www.opengov.go.tz)), **Government Open Data Portal** ([www.opendata.go.tz](http://www.opendata.go.tz)), Tovuti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ([www.utumishi.go.tz](http://www.utumishi.go.tz)) na mitandao yake ya kijamii ya Facebook ([utumishiweek](http://www.facebook.com/utumishiweek)), na Blog (<http://www.utumishiweek.blogspot.com/>).

Serikali inawahimiza Wadau na Wananchi kushiriki kikamilifu kutoa maoni yao. Mwisho wa kupokea maoni, ushauri au mapendekezo toka kwa wadau na wananchi na ni **tarehe 10/09/2016 Saa 09:30 Alasiri**.

Imetolewa na:

A handwritten signature in blue ink, likely belonging to the Minister of the Office of the President.

MPANGO WA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI (OGP)  
02 SEPTEMBER, 2016.